# Dhima ya Kibwagizo katika Ushairi wa Kiswahili

*Clara Momanyi na Joseph N. Maitaria*

*Ikisiri*

Makala haya yanatathmini dhima ya kibwagizo katika ushairi wa Kiswahili. Baadhi ya wahakiki wa utanzu huu wamekuwa wakitoa maelezo ya kijumla kuhusu uwiano uliopo kati ya kibwagizo cha shairi na maudhui yanayowasilishwa. Maelezo hayo yanaibua utata katika fasili na maana ya mshororo huo ujulikanao kama kibwagizo. Hali hii inaonesha kwamba matumizi ya kibwagizo bado hayajashughulikiwa ipasavyo. Katika makala haya, kibwagizo kimefafanuliwa kwa namna kinavyoweza kusaidia kuibua umbo, muundo, kuelekeza mtindo na ridhimu au mahadhi katika ushairi wa Kiswahili. Aidha, makala yanadhukuru namna kibwagizo kinavyoweza kutumiwa katika uainishaji wa mashairi.

## 1.0 Utangulizi

Ushairi wa Kiswahili umekuwa ukitumia kibwagizo kama kipengele muhimu katika utunzi na uwasilishaji wake. Kibwagizo ni mshororo ambao huukariri ujumbe unaowasilishwa katika shairi. Hata hivyo, dhima ya kipengele hiki haijabainishwa wazi katika ushairi wa Kiswahili. Kudai kwamba kibwagizo ni mshororo au chombo kinachobeba maudhui tu ni wazo finyu na huweza kupotosha. Fasili za jumla kama hizi huweza kupotosha hadhira kuhusu matumizi yake katika ushairi. Ni katika muktadha huo ambapo makala haya yanatathmini na kudhihirisha utendakazi au dhima ya kibwagizo katika ushairi wa Kiswahili kwa kuzingatia mifano mahsusi ya mashairi. Aghalabu, tungo nyingi za ushairi wa Kiswahili ambazo huwasilishwa kwa kuzingatia arudhi za kimapokeo, zimekuwa zikitumia kibwagizo kama kipengele cha kimtindo katika kukidhi mahitaji ya mtunzi. Kibwagizo kama mshororo katika shairi, kina idadi maalumu ya mizani na mpangilio wa vina. Halikadhalika, baadhi ya tungo hizo hutumia ukariri wa kibwagizo katika beti zote za shairi husika. Mashairi mengine yamekuwa yakitumia kibwagizo mwanzoni mwa beti (Taz. shairi la 'Ajabu' katika *Sikate Tamaa* la Mohamed (1980) na shairi la 'Mcheza Hawi Kiwete' katika *Wasakatonge* la Khatib (2003). Isitoshe, tungo zingine hutumia kibwagizo kifupi au kirefu sawa na mishororo inayopatikana katika beti husika. Katika muktadha huu inaweza kuakisiwa kuwa matumizi hayo hutegemea jinsi na namna mtunzi anavyotaka kuuwasilisha utungo wake.

## 1.1 Kibwagizo ni nini?

Kibwagizo kama dhana kimetolewa fasili mbalimbali kulingana na namna kinavyojitokeza na kutumiwa katika beti za ushairi wa Kiswahili. Abed (1954), kwa mfano, anasema kwamba kuna istilahi mbalimbali zinazotumika

kufafanulia dhana hiyo hiyo moja kama vile kibwagizo, kiitikio, kipokeo, mkarara na kituo. Nao Syambo na Mazrui (1992) wanasema kwamba mshororo unaorudiwa mwishoni mwa kila ubeti kwa maneno yaleyale huitwa kipokeo au kibwagizo. Maelezo kama haya yanashadidiwa na wahakiki wengine wa ushairi kama vile Masinde (2007), King'ei na Amata (2001) na Mohamed (1990) ambao wanafafanua kwamba kibwagizo ni mstari wa mwisho wa ubeti wa shairi unaorudiwa katika kila ubeti wa shairi, na ambao huitwa pia mkarara, kiitikio au kipokeo (Taz. pia Walibora, 2012).

Kibwagizo ni mstari wa mwisho unaoitikia ujumbe. Aidha, hupatikana katika aina za mashairi kama vile tarbia, takhmisa, tasdisa, ukumi, utumbuizo, ngonjera na malumbano. Huu ni mshororo unaobeba ujumbe muhimu katika shairi. Huitwa kituo ikiwa mstari huo ni kimalizio katika ubeti (Kisia na Mwarandani, 2007 na Ruo, 1989). Kwa ujumla, fafanuzi hizo zinakihusisha zaidi kipengele cha kibwagizo na maudhui yanayoibuliwa. Kwa mujibu wa makala haya, kibwagizo kitachukuliwa kuwa ni mshororo maalumu unaokaririwa na unaojitokeza ama mwanzoni au mwishoni mwa beti ili kuwasilisha ujumbe wa shairi. Kimuundo, kibwagizo ni mshororo ambao una idadi maalumu ya mizani na urari wa vina. Isitoshe, kibwagizo si lazima kiwe na umbo moja muhususi. Aidha, hudhibitiwa na kuwasilishwa kwa miundo ya maneno au kauli teule za lugha ili kuelekeza mtindo katika uwasilishaji wa hisi za mtunzi.

## 2.0 Dhima ya Kibwagizo katika Ushairi wa Kiswahili

Kibwagizo ni dhana ambayo hutumiwa mno kama kipengele maalumu hususan katika uwasilishaji wa shairi la kimapokeo. Hapa ieleweke kuwa hata ule ushairi usiozingatia zaidi arudhi hizo huweza kudhihirisha matumizi ya kibwagizo kwa mitindo isiyokuwa ya wazi. Dhima ya kibwagizo katika ushairi wa Kiswahili inaweza kubainika kupitia njia zifuatazo:

### 2.1 Ukariri wa Mawazo au Ujumbe Unaowasilishwa

Kimsingi, shairi kama sanaa yoyote ya kifasihi, hutungwa ili kuwasilisha ujumbe fulani kwa hadhira. Katika kufanya hivyo, kauli teule hutumiwa ili kuibua mawazo kwa kuzingatia maelezo na mifano mbalimbali. Kwa mantiki hiyo, dhamira aliyo nayo mtunzi kuhusu jambo fulani huweza kubainishwa kupitia kauli hiyo teule. Ujumbe huo wa mtunzi huenda umewasilishwa kimafumbo au kwa mizungu ya tamathali za semi. Kwa hiyo, mbali na kubuni tungo zenye usanifu wa kuvutia, mshairi huwa na nia ya kuuwasilisha ujumbe kwa jamii yake, kwa njia iliyo wazi kupitia ukariri wa kibwagizo.

Kwa kuwa kibwagizo ni fingo la ubeti, kinakuwa pia dira ambayo humrejesha zaidi msomaji katika ujumbe unaozingatiwa. Kuna njia mbalimbali za kuukariri ujumbe katika shairi la Kiswahili. Mtunzi huweza kufanikisha hayo kulingana na jinsi anavyotumia mishororo inayojenga umbo la shairi lake. Kwa mfano, shairi la 'Mhadhari' lililotungwa na Gora Haji Gora katika *Tamthilia ya Maisha* (Wamitila, 2005:45) huweza kubainisha ukariri huo wa ujumbe:

*Anae wacha jamii, inayomuhusu yeye,*
*Na kuifanya rai, kwa kuwa iangamiye,*
*Kwengine nako hafai, lazima umuhofiye,*
*Siji unakaribiye, lazima umuhadhari*

Katika shairi hilo, mshororo wa mwisho wa ubeti huo uliopigiwa mstari umerudiwa katika beti zote za shairi. Mtindo huo wa kurudiarudia mshororo wa mwisho katika kila ubeti hupatikana kwa wingi katika mashairi yanayozingatia arudhi (Taz. mashairi mengi yanayopatikana katika diwani za *Waja Leo* (Walibora, 2012) na *Sauti ya Shangwe* (Babusa, 2011)). Aidha, msanii huweza kutumia ukariri wa mshororo mahali tofauti kukidhi haja hiyo hiyo. Kibwagizo huweza kutumiwa kama kianzio cha beti za shairi. Kwa mfano, shairi la 'Tenda Haki' katika *Malenga wa Ziwa Kuu* (Wallah, 1988:36) linadhihirisha hali hiyo ambapo 'Tenda Haki' ni kibwagizo kinachokaririwa:

*Tenda Haki*
*Ni matendo yake Mungu, Jabari*
*Aliotugawa mafungu, tayari*
*Akatupa ulimwengu, fahari* (Ubeti wa 1)

Kwa kukariri kibwagizo hicho, ujumbe unaowasilishwa huwa umetangulia kudokezwa. Aidha, mada msingi hapa ni kauli inayopatikana katika anwani ya shairi. Mishororo mingine katika ubeti huchangia kuufafanua huo ujumbe unaohusu umuhimu wa kuzingatia haki. Mtunzi hutumia kibwagizo kama mtindo katika kuwasilisha ujumbe wake. Kwa hivyo, hadhira inapaswa kuelewa kuwa ukariri wa kibwagizo ni njia mojawapo ya kuubainisha ujumbe unaowasilishwa katika shairi. Hii pia isichukuliwe kuwa mshairi anapotumia maneno yaleyale au miundo ileile ametindikiwa au kupwelewa katika udhibiti wa msamiati au kauli msingi zinazohitajika. Mtunzi hutumia kibwagizo kama mtindo kwa lengo la kusisitiza ujumbe unaowasilishwa mbali na kuongeza ladha na kudhibiti mahadhi katika shairi lake.

## 2.2. Kibwagizo kama Chombo cha Kujengea Usaili na Tafakuri

Kwa vile kibwagizo ni mshororo muhimu katika beti za shairi, mshairi humtarajia msomaji wake kuzingatia maneno yaliyotumika kwani huweza kuwa kichocheo cha kuibulia usaili na tafakuri zaidi katika ujumbe unaowasilishwa ili kupata maana inayokusudiwa. Shairi huweza kuwa na maana ya juu juu au ya ndani (Wamitila, 2005). Katika muktadha huo, maneno ambayo hutumiwa katika kibwagizo huwa ni yale ambayo yameteuliwa kwa makini kuwa ishara ya kuufikia ujumbe batini uliofundikwa kwenye shairi. Mshairi kwa kawaida hana muda mrefu wa kufaragua kwa kina hoja au ujumbe anaowasilisha kama inavyobainika katika tanzu zingine za fasihi kama vile riwaya. Mshairi huitarajia hadhira yake kushiriki siyo tu katika usomaji tuli bali pia katika kuliajiri bongo ili kuweza kupambanua maana batini iliyosetiriwa katika shairi (Senkoro, 1988). Hoja hii inaweza kufafanuliwa kwa kuzingatia shairi la 'Imani ya Mwana' katika *Sikate Tamaa* (Mohamed, 1980):

> *Kwani mamangu u ng'ombe, au punda wa dobi*
> *Nalia chozi usambe, nayavunja madhehebu*
> *Nalia chozi kikombe, uchungu wanisibi*
>     *Hebu nambie*
> *Kweli jaza ya kiumbe, ni madhila na mapigo*

Katika ubeti huo na katika beti zote za shairi hilo, mishororo hiyo iliyopigiwa mstari ndiyo inayokaririwa. Umbo hilo la kibwagizo, kijuujuu linaonekana kama linalohusisha mishororo miwili, yaani ule mshororo unaosema '*Hebu nambie*' unaokamilishwa na sehemu inayofuatia. Katika muktadha wa kibwagizo hicho, hadhira inahitaji kukichukulia kuwa kichocheo cha usaili na tafakuri. Binadamu anapotenda wema huishia kuteswa? Mazingira hayo hayo yamejengwa pia kwenye shairi la 'Wasafiri Tuamkeni' katika *Sauti ya Dhiki* (Abdalla, 1973:67):

> *Bado safari ni ndefu, wasafiri tusichoke*
> *Natusiwe madhaifu, twendeni hadi tufike*
> *Tusafiri bila hofu, wenye nazo ziwatoke*
> *Huu ndiwo mwanzo wake, siwo mwisho wa safari*

Ubeti huu ni mfano mmojawapo unaodhihirisha namna usaili unavyofumwa na unavyojitokeza katika beti za shairi. Kwanza, usaili unajengwa kwa matao ya chini katika mishororo ya awali na kilele chake hufikiwa kwenye safu ya kibwagizo. Kwa hivyo, hadhira huweza kujiuliza: kwa nini jitihada zilizofanywa kabla, si za kuendeleza bali ni mwanzo na wala si mwisho wa safari? Swali kama hilo huielekeza hadhira kujitafutia mifano mahususi inayotokana na tajiriba au inayotokana na uhalisia wa maisha katika jamii.

Zaidi ya kibwagizo kufumbata maana batini, mshairi hutarajia ujumbe unaowasilishwa uifikie hadhira kusudiwa. Kwa hivyo, hadhira hupata tija ya burudani kupitia mizungu ya kauli na maneno teule yaliyotumika (Abdalla, 1973). Hapa ieleweke kuwa maneno yaliyotumika katika kibwagizo huwa ni matini au ishara zinazohitaji kufasiriwa na kupatanishwa na baadhi ya vipengele vinavyopatikana katika matukio yaliyo au yanayoshuhudiwa katika jamii inayorejelewa (Wafula na Njogu, 2007). Huu ni ushahidi kuwa ushairi wa Kiswahili hufasiriwa vizuri zaidi kupitia kuhusishwa kwake na miktadha mahususi ya jamii.

### 2.3 Kibwagizo kama Mtindo katika Uwasilishaji

Tumebainisha hapo awali kwamba kibwagizo ni mshororo ambao huweza ama kutumiwa kwa ukariri mwanzoni au mwishoni mwa ubeti. Matumizi hayo hutekeleza dhima ya kimtindo katika uwasilishaji wa ushairi wa Kiswahili. Muundo wa kibwagizo huweza kuwa ni mshororo mfupi au mrefu kutegemea mizani iliyozingatiwa katika mishororo mingine ya ubeti. Mfano wa mashairi yaliyotumia kibwagizo mwanzoni ni kama vile shairi la ‘Asasi’ katika *Malenga wa Ziwa Kuu* (Wallah, 1988) na shairi la ‘Ajabu’ katika *Sikate Tamaa* (Mohamed, 1980). Katika *Malenga wa Ziwa Kuu,* Shairi la ‘Asasi’ limewasilishwa ifuatavyo:

*Jenga msingi bora*
*Msingi wa kila jambo, muhimu kuliko mwisho*
*Ndio huleta mapambo, mara ya ukumbusho*
*Ukianza kombokombo, halima kuna vituko*

Katika utungo huu, ‘Jenga msingi bora’ ndicho kibwagizo kinachowekwa mwanzoni mwa kila ubeti wa shairi. Halikadhalika, katika *Sikate Tamaa,* kuna shairi la ‘Ajabu’ ambapo kibwagizo hicho hicho kimetumiwa mwanzoni mwa kila ubeti, kama ifuatavyo:

*Ajabu ajabu hii ajabu*
*Mwenye maneno hasemi*
*Asonayo atasema*
*Na nyuma hawatazami*
*Mbele wamekuandama*

Madondoo hayo yametumia kibwagizo kama mishororo inayorudiwa au kukaririwa katika beti zote katika shairi linalozingatiwa. Mshororo huo ungeweza kuhamishiwa mwishoni mwa beti kama mtunzi angetaka. Huo ni uhuru wa kishairi ambao mtunzi hujipa ili kuweza kuchezea kwa usanifu

mshororo wa kibwagizo. Kimsingi, mtunzi anapotumia kibwagizo mwanzoni mwa ubeti huwa anaielekeza zaidi hadhira yake kwenye maudhui yanayowasilishwa. Hali hii ni tofauti na jinsi kinavyotumika mwishoni mwa beti ambapo huwa ni fingo la shairi. Kwa kuzingatia mtindo huo, mshairi hudhihirisha uhodari wake katika usarifu wa kibwagizo.

Mtindo wa matumizi ya kibwagizo hudhihirika pia wakati ambapo mshororo wa mwisho katika ubeti haurudiwi kwa umbo moja, yaani umbo hilo hilo. Jambo hili ndilo lililowaelekeza baadhi ya wahakiki kuchukulia kuwa dhana ya kibwagizo huweza kufafanuliwa kupitia istilahi mbalimbali kama vile kiitikio, mkarara, kipokeo au kituo (Abed, 1973). Hapa tutatofautisha kidogo istilahi hizo katika muktadha wa ushairi wa Kiswahili kama ifuatavyo: **Kituo** ni mshororo wa mwisho katika ubeti ambapo maneno yaliyotumika yanaweza kutiririshwa katika beti zote. Ikitokea hivyo itakuwa pia ni **kibwagizo**. Ikiwa maneno hayo hayakutiririshwa katika beti zote – yaani mishororo ya miisho ya beti ni tofauti basi ni **kimalizio**. **Kibwagizo** ni mshororo wa mwisho wa ubeti ambao hukaririwa katika beti zote za shairi. Pia, huweza kuitwa *Mkarara* au *Kiitikio* iwapo shairi linanuiwa kughanwa au kusomwa kimoyomoyo.

Mifano tuliyotoa inadhihirisha kuwa kuna mitindo mbalimbali ya kutumia kibwagizo. Shairi ambalo lina kibwagizo hughanwa au husomwa kwa mtindo mmoja. Halikadhalika, shairi ambalo lina kimalizio au kituo tofauti, beti zake huweza kusomwa kwa mahadhi tofauti tofauti mbali na kuwepo kwa tofauti za kimaumbo. Sababu muhimu ya kufanya hivyo ni mshairi kutotaka kuichosha hadhira katika usomaji. Kwa maelezo hayo fasiri ya kibwagizo si ya moja kwa moja na huenda ikazua utata. Utata huo unaweza kudhihirishwa kupitia kwa shairi la ‘Rangi Hii’, katika *Kina cha Maisha* (Mohamed, 1984):

*Vitu ‘ikuki vilivyo vimepakwa rangi*
*Si mno*
*Viishivyo na visivyo vilivyorembwa kwa wingi*
*Si mno*
*Mno ni rangi ya ngozi*

Katika ubeti huu na katika beti zote za shairi hilo, mishororo hiyo iliyopigiwa mstari imekaririwa. Maneno ‘si mno’ yamerudiwa mara mbili katika kila ubeti. Huo ni mtindo unaotumika zaidi katika mashairi ya Kiswahili yasiyozingatia arudhi katika uwasilishaji wake.

## 2.4 Matumizi ya Kibwagizo katika Kuelekeza Mahadhi

Kutokana na mpangilio mahususi wa maneno, shairi huweza kusomwa au kughanwa kwa mahadhi na ridhimu tofauti tofauti. Kwa mfano, urari wa mizani na mpangilio wa vina husababisha shairi kusomwa kwa mapigo ya sauti ya

kimuziki. Kwa hivyo, maneno yanayotumiwa katika upatanisho wa vina husaidia kuunda toni au lahani ya shairi (Mulokozi na Kahigi, 1979). Mshairi hufunga mianya yote ya usomaji ila kwa uelekezi wa jinsi mizani na vina vilivyotumika. Kwa vile kibwagizo ni mshororo muhimu, athari yake huhisika katika beti na shairi zima kwa ujumla. Kwa mfano, endapo ujumbe unaowasilishwa utakuwa ni wa furaha, shairi hilo litasomwa kwa kasi hadi inapofika kwenye kibwagizo ambapo msomaji au msikilizaji anaathiriwa kihisia na yale yanayosisitizwa. Mfano wa shairi lenye ujumbe huo wa furaha ni kama hili liitwalo 'Pokea Barua' kutoka katika *Diwani ya Jinamizi* (Zakwany, 1979:56). Mshairi anatongoa:

> *Nakupenda muadhamu, mzuri wa kuumbika*
> *Sili sipati naumu, moyo umeswalitika*
> *Hasa ukitabasamu, nazidi kuazirika*
> *Nipe saa na dakika, tukutane muadhamu*

Kibwagizo cha shairi ni huo mshororo wa mwisho uliopigiwa mstari. Maudhui yanayowasilishwa si mazito na kutokana na matarajio ya kuanzishwa kwa usuhuba, shairi linaweza kusomwa kwa kasi ambapo kilele chake ni kibwagizo. Shairi hilo linazua hisia tofauti likilinganishwa na shairi la 'Kuondokewa' na P'Bitek' katika *Miale ye Uzalendo* (King'ei, 2000), ambalo limejengeka katika mazingira ya huzuni:

> *Mhariri nakujia, mna kilio moyoni*
> *Jamii yote twalia, sasa tutafanya nini*
> *Limetufika tanzia, la ndugu yetu yakini*
> *Tunamwombea manani, amlaze mahali pema*

Katika mazingira ya huzuni, ubeti huo hutarajiwa kusomwa pole pole kuanzia mwanzo hadi kilele chake ambacho ni kibwagizo. Hivyo, hali, toni na mwendo hubadilika. Kama ilivyoelezwa hapo awali, mtunzi huwa na kichomi fulani ambacho hudhihirika katika shairi kupitia kwa miundo teule ya lugha ya uwasilishaji. Mazingira ya hisi ya msanii hudokezwa katika mishororo ya awali ya beti za shairi lakini athari yake hukita zaidi katika kibwagizo.

Iwapo kibwagizo kinachozingatiwa ni mshororo wa mwisho katika ubeti, msomaji atausoma kwa msisitizo wa toni kuliko ile mishororo iliyotangulia. Halikadhalika, kibwagizo kikiwa mwanzoni mwa ubeti mshororo huo utasomwa kwa mshindo zaidi kuliko ile mingine inayofuatia katika ubeti. Suala la hali, toni na mwendo hubainika kupitia kwa viakifishi, urari wa mizani na mpangilio wa vina. Ieleweke pia hapa kwamba sio lazima kila shairi liwe na kibwagizo. Shairi huweza kukosa kibwagizo na hili humtegemea mshairi

mwenyewe. Msanii asipozingatia kibwagizo, huzingatia nyenzo zingine zinazoibua mahadhi na ridhimu kama vile urari wa mizani na mtiririko wa vina. Kutotumia kibwagizo huweza pia kutokana na aina ya shairi linalowasilishwa.

**3.0 Hitimisho**

Makala haya yametathmini matumizi ya kibwagizo katika muktadha wa ushairi wa Kiswahili. Imebainishwa kuwa ingawa kibwagizo kina dhima ya kuukariri ujumbe, ichukuliwe kwamba kipengele hiki ni miongoni mwa vipengele muhimu, hususan katika mashairi ya kimapokeo. Aidha, kibwagizo ni dira ya kubainisha ufundi wa lugha katika uwasilishaji. Katika makala haya imeelezwa kupitia mifano kwamba, kuna baadhi ya mashairi ambayo yamekiuka ule ukawaida wa kuwa na kibwagizo mwishoni mwa kila ubeti wa shairi. Kibwagizo huweza pia kuwa kianzio cha ubeti ambapo huwa mshororo wa awali katika ubeti. Makala haya pia yamedurusu dhana ya kibwagizo katika ushairi na kuafiki kwamba ni mshororo wowote ambao ni angavu zaidi katika ubeti au shairi zima kwa ujumla. Kutokana na umuhimu wake basi, kibwagizo huweza kukaririwa kwa muundo huo huo au kukaririwa kiusambamba.

## Marejeo

Abdalla, A. (1973). *Sauti ya Dhiki.* Nairobi: Oxford University Press.
Abed, K. A. (1954). *Sheria za Kutunga Mashairi.* Nairobi: East African Literature Bureau.
Babusa, H. S. (Mh.) (2011). *Sauti ya Shangwe.* Mombasa: Chesil Printers.
Khatib, M. S. (2003). *Wasakatonge.* Dar es Salaam: Oxford University Press.
King'ei, K. (2000). *Miale ya Uzalendo.* Nairobi: Phoenix
King'ei, K. na K. Amata. (2001). *Taaluma ya Ushairi.* Nairobi: Acacia Stantex Publishers.
Kisia, A. na B. Mwarandani. (2007). *Ukero wa Ushairi kwa Shule za Upili Ukijumlisha Utungo wa Diwani Yetu.* Nairobi: Kenya Literature Bureau.
Masinde, E. W. (2007). *Ufundishaji wa Ushairi katika Shule za Upili na Vyuo.* Eldoret: Taaluma Publishers.
Mohamed, S. A. (1980). *Sikate Tamaa.* Nairobi: Longhorn Publishers Ltd.
Mohamed, S. A. (1984). *Kina cha Maisha.* Nairobi: Longman Kenya Ltd.
Mohamed, S. A. (1990). *Mbinu na Mazoezi ya Ushairi.* Nairobi: Evans Brothers Kenya Ltd.
Mulokozi, M. M na K. K. Kahigi. (1979): *Kunga za Ushairi na Diwani Yetu.* Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.
Ruo, K. R. (1989): *Nguzo za Ushairi wa Kiswahili.* Nairobi: Macmillan Publishers Ltd.
Senkoro, F. E. M. K. (1988). *Ushairi na Nadharia ya Tahakiki.* Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.
Syambo, B. K. na A. Mazrui. (1992). *Uchambuzi wa Fasihi.* Nairobi: East African Educational Publishers.
Wafula, R. M. na K. Njogu. (2007). *Nadharia za Uhakiki na Fasihi.* Nairobi: The Jomo Kenyatta Foundation.
Walibora, K. (Mh.) (2012). *Waja Leo.* Nairobi: Oxford University Press.
Walla, W. (1988). *Malenga wa Ziwa Kuu. Maswali na Istilahi za Kifasihi.* Nairobi: East African Educational Publishers Ltd.
Wamitila, K. W. (Mhr.) (2005): *Tamthilia ya Maisha.* Nairobi: Vide-Muwa Publishers Ltd.
Zakwany, A. S. (1979): *Diwani ya Jinamizi.* Nairobi: Shungwaya Publishers Ltd.